



Hadithi ya Agostino

História do Agostino

- ✎ LIDA Italia
- ⌚ Billie Cejka Risnes
- 💬 Jacob Haule
- 🔊 5
- 💬 Kiswahili sw / português pt



Ninaitwa Agostino na nina umri wa miaka 51. Kazi yangu ni kusambaza chakula kwa balskeli. Nina mabinti wawili, lakini ninaongea nao mara chache sana. Mimi na mama yao hatuishi pamoja tena kwa sababu tumeachana.

...

O meu nome é Agostino e tenho 51 anos. O meu trabalho é fazer entregas de comida, em bicicleta. Tenho duas filhas, mas raramente falamos. Eu e a mãe delas já não vivemos juntos porque nos divorciámos.



Ninaishi na mama yangu kwa sababu siwezi kumudu kulipa kodi ya nyumba baada ya kuachana. Kodi ya nyumba ni gharama kubwa sana katika jiji hili.

...

Vivo com a minha mãe, porque depois do divórcio, não consigo pagar uma renda. Nesta cidade, a renda é muito cara.



Miezi michache iliyopita, nilikuwa nikifanya kazi kama bawabu katika kampuni. Nilitengeneza vitu vilivyo haribika, nilibeba maboksi, na nilimsaidia yeyote aliye hitaji msaada. Siku moja, kampuni ilinifukuza kazi. Sikujua ni kwa nini.

...

Há alguns meses eu trabalhava como zelador para uma empresa. Reparava coisas que estivessem partidas, carregava caixas e ajudava quem precisasse. Um dia a empresa despediu-me. Não comprehendi porquê.



Niliwaona watu wengi wakileta chakula kwa baiskeli. Ninaweza kuendesha baiskeli, kwa hiyo niligonga mlango wa kampuni kubwa ya usambazaji. Walinipa yuro tatu kwa kila safari. Ninaingiza yuro 40 kwa siku, yuro 60 nikibahatika sana, na wateja wananiongezea.

...

Vi muitas pessoas a fazer entregas de comida em bicicleta. Eu sei andar, então bati à porta da empresa de entregas. Ofereceram-me três euros por cada entrega. Faço 40€ por dia, 60€ se tiver muita sorte e os clientes me derem uma gorjeta.



Sipati likizo ya malipo, hakuna malipo ya kuugua, na haki mbalimbali kwa ujumla. Sidhani kama hii ni sawa, lakini ninahitaji kazi. Waajiriwa wengi ni wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali duniani.

...


Não tenho férias pagas, ou baixa médica, e quase nenhum direito. Penso que isso não está certo, mas eu preciso do emprego. A maioria dos trabalhadores são imigrantes de todo o mundo.



Watu wengi wanaofanya kazi ya usambazaji wanaumia katika ajali kila siku. Baadaye, wakati kijana wa miaka 25 anayefanya kazi hii alipogongwa na gari na akafa, mamlaka zikaanza kututambua. Ni aibu kwa sababu hili lilitokea baada ya yeye kufariki.

...

Todos os dias, muitas pessoas que fazem entregas sofrem acidentes. Quando um homem de 25 anos que fazia entregas foi atropelado por um carro e morreu, as autoridades começaram a reparar em nós. Foi uma pena que ele tivesse morrido antes de isso acontecer.



Kwa kushirikiana na madereva wengine wa usambazaji kutoka katika makampuni mengine, nilisoma kozi inayohusu haki za wafanyakazi katika chama fulani nchini. Walitupa ushauri wa kisheria bure kabisa. Tukapambana ili tutambulike na tupate haki zaidi.

...

Juntamente com outras pessoas que fazem entregas, de outras empresas, fiz um curso em direitos dos trabalhadores no sindicato local. Ofereceram-nos conselhos legais gratuitos. Temos dificuldade em obter mais reconhecimento e direitos.



Baada ya muda mrefu, jitihada zetu zikazaa matunda. Kampuni moja kubwa ya usambazaji ililazimika kulipa faini kubwa na kuwapa wafanyakazi wake ajira za kudumu. Ilikuwa ni mara ya kwanza jambo kama hili kutokea duniani. Inaonekana kama mambo yameshaanza kuboreshwa.

...

Depois de muito tempo, todo o nosso trabalho árduo valeu a pena. Uma grande empresa de entregas teve de pagar uma multa enorme e de dar aos trabalhadores empregos permanentes. Foi a primeira vez que isso aconteceu em qualquer parte do mundo. Parece que as coisas estão a começar a melhorar.



LIDA Stories

lidastories.net

Hadithi ya Agostino

História do Agostino

✍ LIDA Italia

✉ Billie Cejka Risnes

☞ Jacob Haule (sw), Marta Pinto (pt)

